
لا إله إلا الله محمد رسول الله

# ZAKAT

## NA

# SAUMU YA RAMADHANI



**JUMUIYA YA WAISLAMU**
**WAAHMADIYYA TANZANIA**
**S.L.P. 376**
**DAR ES SALAAM**

# ZAKAT

***Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.***

ZAKAAT kwa Kiarabu ni neno lenyc maana mbili: (1) kuongezeka, na (2) kutakasika. Katika sheria ya Kiislamu maana yake ni kutoa sadaka sehemu maalumu ya Mali liyoichuma Mwislamu kwa njia ya halali.
Kutoa Zaka ni nguzo ya nne katika nguzo tano za Kiislamu; na kila Mwislamu, mwanamume au mwanamke, akiwa na kipimo maalumu cha mali, amelazimishwa kuitoa. Zaka imetajwa pamoja na Sala ndani ya Kurani Tukufu na hilo laonyesha jinsi ilivyo muhimu amri hii. Mwenyezi Mungu alimwamrisha Mtume Muhammad s.a.w. kuchukua sadaka kwa Waislamu.
Akasema “Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe kwayo na kuwatakasa, na uwaombee. Hakika kuomba kwako ni utulivu kwao; na Mwenyezi Mungu ndiye Asikiaye, Ajuaye.” (9:103).
Baada ya kufariki Mtume s.a.w. Makhalifa wake waliendelea kupokea sadaka hiyo kwa Waislamu, na wakati mmoja baadhi ya Waislamu walipokataa kutoa Zaka, Seyidna Abu Bakr, Khalifa wa kwanza wa Mtume, Mungu awe radhi naye, akawa tayari kupigana nao, akatangaza kwamha hataacha kuwapiga vita watu hao mpaka watoe kile kipande cha kamba cha kufungia goti la ngamia walichokuwa wakitoa zama za Mtume s.a.w. Maana yake, Mwislamu ambaye anayo mali wala hatoi sehemu yake iliyolazimishwa na Mwenyezi Mungu hawi Mwislamu tena
Tena amesema Mwenyezi Mungu, "Na kama wakitubu na kusimamisha Sala na kutoa Zaka, basi ni ndugu zenu katika dini" (9:11). Bila shaka kutoa Zaka kunaimarisha udugu wa Uislamu, na mwenye kuitoa tu ndiye ndugu ya Waislamu wengine.

**HAKI YA MASKINI**
Juu ya sadaka hii Mtume s.a.w. alisema kuwa “Zaka inachukuliwa kwa matajiri wa Waislamu na hurudishiwa mafukara wao”.
Neno la "kurudishiwa" linastahili kufikiriwa kidogo. Mtume s.a.w. hakusema "hupewa" bali alisema "hurudishiwa". Mradi wake ni kwamba watu wanaopewa sehemu katika Zaka hawafanyiwi hisani na wenye kuitoa, bali kwa hakika wanapokea haki yao.

N.B. Hadithi zilizomo katika kitabu hiki zimechukuliwa ndani ya KASHF-UL-GUMAH.

Fundisho hili ni la maana sana. Inaonekana kuwa katika dini ya Kiislamu vitu vyote vilivyomo duniani vimeumbwa kwa ajili ya wanadamu wote kwa jumla. Kurani Tukufu imesema.
"Na Amekutiishieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini vyote vimetoka Kwake" (45:14). Tena amesema, "Na ambao katika mali zao iko sehemu maalumu kwa ajili ya aombaye na anayezuilika kuomba" (70:25,26): Basi mtu anayechuma mali, hiyo yote si yake peke yake; bali iko ndani yake haki ya watu wengine. Kwa maana ardhi na mvua na wanyama na madini na vyombo vingine vya kuchumia mali, kwa hakika, viliumbwa kwa ajili ya wanadamu wote. Basi tajiri anayechuma mali kwa kutumia vile vitu vilivyoumbwa si kwa ajili yake tu awe na hakika ya kuwa haki ya watu wengine haikosi kuwamo katika mali yake. Na asipotoa haki ya watu hao mali yale hayatakuwa halali kwake. Ndiyo sababu neno lililotumiwa kwa sadaka hiyo ni "zaka", yaani kitu cha kutakasa mali. Kwa maneno mengine, mali aliyopata mtu haiwi halali kwake mpaka awe ametoa sehemu maalumu kwa ajili ya watu wengine ambayo ni haki yao.

**NJIA ZA KUTUMIA ZAKA**
Kurani Tukufu imetaja njia nane za kutumia Zaka: (1) Kuwapa mafukara, watu ambao umaskini wao umeonekana waziwazi:
(2) Maskini, ambao wameishiwa mali au njia za kuchumia mali lakini wanajaribu kuuficha umaskini wao wasiudhihirishe kwa wengine kwa sababu ya ari ya moyo wao; (3) Wafanyao kazi ya kukusanya Zaka, wawe masharifu au masheikh au watu wengine wo wote wafanyao kazi hiyo: (4) Waungiwao mioyo yao, yaani watu ambao nyoyo zao zimeelekea kwenye dini,

lakini kwa kuwa wametengana na jamaa zao, wanakuwa na haja ya msaada.
Hiyo siyo maana yake kwamba watu wapewe fedha na kuvutwa kuingia dini ya Islamu, bali watu wapya katika dini ambao pengine wanaachishwa kazi au wanataabishwa kwa njia nyinginezo kwa sababu ya wao kuacha dini yao ya zamani na kukubali dini ya Islamu wamewekewa sehemu katika mali ya Waislamu.
(5) Kuwakomboa wafungwa na watumwa. Wale watu ambao wanafungwa kwa kutoweza kulipa deni pia wanaweza kusaidiwa na pesa hizo. Hata wafungwa na watumwa wasiokuwa Waislamu wanaweza kukombolewa na kuachwa huru kwa fedha ya Zaka (6) Wasio na uwezo wa kulipa madeni yao au walipata hasara; nzito katika biashara zao au waliotakiwa kulipa dia (gharama ya kuua mtu) ya jamaa zao; (7) Katika njia ya Mwenyezi Mungu: katika fungu hili yanaingia matumizi yote yanayofanywa kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu au kwa ajili ya watu wote kwa jumla; kama kueneza na kupigisha chapa vitabu na magazeti ya dini, kufungua shule za elimu za dini na za kidunia, kuendesha hospitali na viwanda vya sanaa na mambo mengine yote yenye kustawisha Waislamu na dini yao; (8) Wasafiri wanaopata taabu katika safari kwa kupungukiwa pesa au wanaosafiri kutafuta elimu. Msafiri ye yote awe tajiri au maskini anaingia katika fungu hili. Nyumba za wageni zaweza kujengwa kwa fedha ya Zaka. Wasio Waislamu pia wanaweza kualikwa waje watembelee nchi za Waislamu na kuonana nao wakalipwa kwa fedha ile.
Matumizi ya Zaka yana wasaa mwingi na watu wote wanapata faida. Siku za Makhalifa wa Kiislamu Mayahudi na maskini wengine wa dini zingine walikuwa wakipata msaada mwezi hata mwezi katika beit-il-mal ya Waislamu. Watu walioshindwa kujipatia riziki kwa sababu ya uzee au ugonjwa au kwa kukosa njia za kuchumia mali walisaidiwa na Makhalifa wa Mtume s.a.w. kwa njia ya Zaka.
Njia hizi nane zilizotajwa na Mwenyezi Mungu ndiyo maelezo hasa ya namna sadaka hiyo inavyotakiwa kutumiwa. Lakini si lazima wasaidiwe kila kundi kwa mpango uliotajwa katika Kurani Tukufu. Imeruhusiwa kutumia fedha yote ya Zaka hata kwa ajili ya haja moja tu iliyo muhimu sana. Kama siku hizi elimu inatakiwa sana na watoto wa Kiislamu, basi ni haki kutumia Zaka kwa kuelimisha watoto wa Kiislamu. Au pengine dini inaweza kulindwa kwa mapato ya Zaka ikionekana imeshambuliwa sana na maadui zake.

## HASARA KWA WAISLAMU

Hasara waliyoipata Waislamu kwa kughafilika kutekeleza faradhi hii haielezeki. Labda walidhani kwamba kwa kujizuia kutoa mali watapata utajiri mkubwa. Lakini baada ya miaka mingi ya mazoea tumeona ya kuwa umaskini umewazidi sana. Katika elimu wao ndio wamekuwa wenye kubaki nyuma kabisa. Katika kazi za serikali wao ndio wamesahauliwa kabisa. Biashara ambayo ilikuwa sababu mojawapo ya ustawi wa Uislamu imetoka mikononi mwao na wameanguka chini pamoja na dini yao. Ujinga, umaskini na magonjwa yamewazinga Waislamu. Upendo uliokuwa ndio alama ya Uislamu hauonekani kati yao. Maskini wanawachukia matajiri na wenye mali wanawaepa wasio nayo.
Hayo ni matokeo ya kuitupilia mbali nguzo hii kubwa ya Uislamu na kwa kuacha kutoa Zaka Waislamu wamenyimwa maombi na baraka za Mtume Muhammad s.a.w. na wafuasi wake wema. Laiti Waislamu wangezinduka na kuhakikisha kwamba unyonge wao na umaskini umeletwa na kughafilika kwao wenyewe.
Mwenyezi Mungu hakuwadhulumu bali wamejidhulumu wenyewe.
Mwislamu halazimishwi kutoa Zaka katika mali kidogo. Kuna kipimo maalumu cha kila kitu, ambacho huitwa nisabu.
Kipimo hicho kikifikiwa inamlazimu Mwislamu kutoa kiasi fulani. Zaka hutolewa kwa ng'ombe, mbuzi na kondoo, ngamia, nafaka zote, tende na zabibu, fedha na dhahabu na bidhaa.

## NISABU YA NG'OMBE

Ng'ombe wakiwa chini ya 30 hawatolewi Zaka.
Kutoka 30 mpaka 39 atatolewa ndama mmoja wa umri wa mwaka mmoja.
kutoka 40 mpaka 59 atatolewa ndama mmoja wa umri wa miaka miwili.

Kutoka 60 mpaka 69 watatolewa ndama wawili wa umri wa mwaka mmoja mmoja.
Kutoka 70 mpaka 89 atatolewa ndama mmoja wa umri wa mwaka mmoja na ndama mmoja wa umri wa miaka miwili.
Kutoka 90 mpaka 99 watatolewa ndama 3 wa umri wa mwaka mmoja mmoja.
Kwa ng'ombe 100 watatolewa ndama 2 wenye umri wa mwaka mmoja na ndama mmoja mwenye umri miaka 2.
Wakizidi hapo ndama mmoja wa umri wa mwaka mmoja atatolewa kwa ng'ombe 30 na ndama mmoja wa umri wa miaka miwili kwa ng'ombe 40.
Ng'ombe wanaofanya kazi shambani hawahesabiwi pamoja na wale wanaotozwa Zaka.

**NISABU YA MBUZI NA KONDOO**
Wakiwa chini ya 40 hakitolewi kitu cho chote.
Kutoka 40 mpaka 120 Mbuzi mmoja
Kutoka 121 mpaka 200 Mbuzi wawili
Kutoka 201 mpaka 300 Mbuzi watatu
Wakizidi hapo mbuzi mmoja atatolewa kwa kila mia moja.
Mbuzi na kondoo wanahesabiwa pamoja. Kwa mfano wakiwa mbuzi 20 na kondoo 20, atatolewa mbuzi au kondoo mmoja.

**NISABU YA NGAMIA**
Wakiwa chini ya 5 hawana Zaka.
Kutoka 5 mpaka 9 Mbuzi mmoja
Kutoka 10 mpaka 14 Mbuzi wawili
Kutoka 15 mpaka 19 Mbuzi watatu
Kutoka 20 mpaka 24 Mbuzi wanne
Kutoka 25 mpaka 35 Ngamia mmoja wa mwaka mmoja
Kutoka 36 mpaka 45 Ngamia mmoja wa miaka miwili
Kutoka 46 mpaka 60 Ngamia mmoja wa miaka mitatu
Kutoka 61 mpaka 75 Ngamia mmoja wa miaka minne
Kutoka 76 mpaka 90 Ngamia 2 wa miaka 2
Kutoka 91 mpaka 120 Ngamia 2 wa miaka 3 kila mmoja
Wakizidi kiasi hicho ngamia mmoja wa miaka 2 atatolewa kwa ngamia 40 na ngamia mmoja wa miaka 3 kwa ngamia 50.

**NISABU YA NAFAKA**
Nafaka zote kama ngano, mpunga, mahindi, mtama, kunde, maharagwe, choroko, wimbi, mawele na nyinginezo kama hizo nisabu zao ni ratili 1,600 au kilo 800. Zikipatikana kiasi hicho au zaidi yake, Zaka itatolewa 1 kwa 10, yaani sehemu ya kumi ya mavuno yote; ila maji yakinunuliwa sehemu ya ishirini ya mavuno italazimu kutolewa.
Asali na tende na zabibu pia hutolewa kwa hesabu ya 1 kwa 10. Zaka ya nafaka inafaa kutolewa mara baada ya kuvuna. Haitakiwi kungoja mwaka upite juu yake. Vitu vingine vidogo vidogo ambavyo hupandwa kwa matumizi ya nyumbani kama mboga za namna mbalimbali na matunda hapana Zaka juu yao.

**NISABU YA FEDHA NA BIDHAA**
Fedha inapotosha ratili moja na wakia 5 na ikapitiwa na mwaka mzima inalazimu kutoa sehemu ya $2^1/_2$ kwa mia yaani sehemu ya arobaini. Kiasi cha dhahabu kinachoweza kununuliwa kwa bei ya fedha ile kinastahili Zaka. Fedha inayowekwa ndani ya banki ikitosha Shs. 100 inatolewa Zaka.
Mapambo ya wanawake ya dhahabu na ya fedha ambayo hayakutumiwa kwa mwaka mzima au yalitumiwa kidogo tu, wala wanawake maskini hawakupewa kuyatumia, yanastahili kutolewa Zaka.
Watu wa biashara waanze kuhesabu tangu walipopata bidhaa inayofikia nisabu, na baada ya

mwaka mmoja kwisha watatoa Zaka juu ya kipimo kilichofika bidhaa yao. Njia iliyo rahisi ya kufanya hesabu ni kama hivi. Kwenye mwanzo wa mwaka tuseme mtu fulani aliagiza vifaa vya Sh. 250/-. Baada ya miezi miwili kupita aliagiza bidhaa nyingine kwa Sh. 20/-. Tena baada ya miezi miwili aliagiza vitu vya Sh. 500/- Basi atafanya hesabu yake kama hivi:

250 x 12 = 3000 Sh. 7200 zitagawanywa kwa 12 ambayo
20 x 10 = 200 itaonyesha wastani wa fedha aliyotumia kwa
500 x 8=4000 mwezi mmoja. Hiyo ni Sh. 600/-. Na sehemu yake ya 40 ni Sh. 15/-. Ndiyo Zaka atakayo-
770 7200 toa kwa bidhaa hiyo. Basi kila mwaka atafanya vivi hivi.

Fedha ambayo mtu anamkopesha mwenzake kwa mwaka mzima au sehemu kubwa ya mwaka haitolewi Zaka, maana yeye hakuitumia. Mwenye kukopa ikiwa amekopa kwa kutimiza haja yake fulani pia hatatoa kitu. Naam, ikiwa aliikopa kwa kufanya nayo biashara, basi atatoa Zaka yake kama kawaida.
Biashara ya vitu vyote hufanywa hesabu yake namna hiyo na kutoa Zaka kama ilivyoelezwa hapo juu. Biashara inayofanywa kwa ushirika Zaka yake itatolewa kwa jumla. Mtume s.a.w. alikataza kutenga mbalimbali fedha au mali au wanyama kwa kuogopa Zaka. Basi haijuzu kuepuka Zaka kwa kila mtu kutenga mbali sehemu yake.
Majengo yaliyojengwa kwa ajili ya biashara kama maduka na fanicha zilizowekwa humo hazina haja kutolewa Zaka. Maana ni vitu vinavyotumika katika biashara. Naam, kama mtu anafanya biashara ya fanicha, yaani anauza viti na meza na masofa au anajenga majumba kwa kuyakodisha na kupata faida yake, basi yeye atafanya hesabu ya bidhaa yake kama kawaida.
Wanaolima katani au kahawa vile vile watafanya hesabu ya mapato yao na kutoa sehemu ya Mwenyezi Mungu sawasawa. Wenye kupanda njugu na ufuta pia watoe sehemu ya kumi, yaani pishi moja katika pishi 10.
Wanaoendesha biashara ya ufugaji wa kuku watafanya hesabu ya mapato yao kama watu wa biashara nyingine.

**MAS'ALA MBALIMBALI**

(1) Zaka inamlazimu kila Mwislamu hata wanawake na watoto. Mtoto anayerithi mali kwa wazazi wake ikiwa mali ile imefikia nisabu, yaani kipimo kilichowekwa na sheria, atatoa Zaka kama kawaida.
(2) Mwehu au majununi aliye na mali mengi atatakiwa kutoa Zaka.
(3) Mfungwa pia atatoa Zaka ya mali yake. Wasimamizi wa mali yake ndio watatoa sehemu ya Zaka mintarafu ya aliyefungwa.
(4) Wakulima hutoa Zaka mara wanapopata mavuno na inatakiwa itolewe kabla ya kuyapeleka ghalani au nyumbani.
(5) Zaka ni sadaka iliyo faradhi. Kuna sadaka nyingine za namna mbalimbali zinazotakiwa kutolewa kwa mahitaji ya namna namna ya taifa la wanadamu.
(6) Hapana Zaka juu ya farasi, punda na nyumbu.
(7) Mnyama mwenye mimba asichukuliwe kwa Zaka, wala asichaguliwe mnyama aliye na faida sana kwa wenyewe, kama ng'ombe wa maziwa; na wanyama waliochoka pia wasitolewe sadaka.
(8) Zaka ya tende na zabibu ni mara moja tu. Ikiisha tolewa mara ya kwanza basi hata vikiwekwa miaka mingapi hapana Zaka tena juu yao. Fedha na wanyama hutolewa Zaka kila mwaka kwa kufanya tena hesabu ingawa wanyama hao walikwisha tolewa Zaka mwaka uliopita.
(9) Mnyama aliyekwisha tolewa sadaka, mtoaji asimnunue tena kwa bei yoyote. Ndiyo sheria juu ya kitu kilichotolewa wakfu au hiba katika njia ya Mwenyezi Mungu.

**AMRI YA KUTOA ZAKA**

Mtume s.a.w. aliamrishwa na Mwenyezi Mungu: "Chukua sadaka katika Mali zao, uwasafishe kwayo na kuwatakasa, na uwaombee. Hakika maombi yako ni utulivu kwao; na Mwenyezi Mungu ndiye Asikiaye, Ajuaye" (9:103).

**MATUMIZI YA ZAKA**

"Sadaka, ni kwa mafukara tu na maskini na wanaozitumikia na waungiwao mioyo yao na kwa (kuwakomboa) wafungwa na wenye deni na katika njia ya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye hekima" (9:60).

**MANABII NA WATU WA ZAMANI WALIAMRISHWA KUTOA ZAKA**

"Na (kumbukeni) Tulipofunga ahadi na wana wa Israeli: . . . simamisheni Sala na toeni Zaka" (2:84).

(2) "Na bila shaka Mwenyezi Mungu Alifunga ahadi na wana wa Israeli: na Tukainua miongoni mwao masultani kumi na mbili. Na Mwenyezi Mungu akasema. Kwa yakini Mimi ni pamoja nanyi. Kama mkidumu katika Sala na mkitoa Zaka" (5:13).

(3) Seyidna Isa (a.s.) alisema, "Hakika mimi ni Mtumishi wa Mwenyezi Mungu; . . . na Ameniusia Sala na Zaka maadamu ningali hai" (16:31,32).

(4) Seyidna Isman (a.s.) alikuwa akiwaamuru watu wake Sala na Zaka" (19:56).

(5) Wazao wa Nabii Ishaka (a.s.) "Tukawafunulia kuzifanya heri na kusimamisha Sala na kutoa Zaka" (21:74).

6) Watu wa Kitabu "Hawakuamrishwa ila kumwabudu Mwenyezi Mungu kwa kumhalisishia dini kwa haki na kusimamisha Sala na kutoa Zaka" (98:6).

**ALAMA YA WANAFIKI**

(1) “Na miongoni mwao yuko anayekusingizia katika sadaka. Na wapewapo katika hiyo huridhika; na kama wasipewe katika hiyo, ndipo wanakasirika" (9:58).

(2) "Sema: Toeni (mali yenu) kwa kupenda au kwa kutopenda, haitakubaliwa kwenu. Hakika ninyi ni watu waasi. Na haikuwazuia ikubaliwe kwao michango yao, ila ya kwamba walimkataa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala hawafiki kusali ila huwa wavivu. Wala hawatoi ila huwa wamechukia. (9:53, 54).

(3) Na katika mabedui yuko anayefikiri ya kuwa anayoyatoa ni gharama ya bure na anawangojeleeni misiba. Msiba mbaya uko juu yao; na Mwenyezi Mungu Ndiye Asikiaye, Ajuaye. (9:98).

(4) Hao ndio wanaosema; Msitoe mali kwa wale walioko kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu mpaka waondoke. Na hazina za mbingu na ardhi ni za Mwenyezi Mungu, lakini wanafiki hawafahamu. (63:8).

**MAKAFIRI PIA HUTOA MALI**

Hakika wale waliokufuru hazitawafaa mali zao wala watoto wao hata kidogo mbele ya Mwenyezi Mungu; na hao ndio watu wa Motoni. Mfano wa vile wanavyovitoa katika maisha haya ya dunia ni kama upepo ambao ndani yake mna baridi kali; ukasibu shamba la watu waliodhulumu nafsi zao na ukaliangamiza; na Mwenyezi Mungu Hakuwadhulumu, bali wao wenyewe wanadhulumu nafsi zao. (3: 117, 118).

**PENGINE HAWATOI**

Na wanapoambiwa: Toeni katika yale Aliyowapeni Mwenyezi Mungu, wale waliokufuru huwaambia walioamini; je, tumlishe ambaye Mungu Akipenda Atamlisha? Nyinyi hammo ila katika upotevu dhahiri. (36:48).

**AMRI YA KUTOA SADAKA**

Ambao huyaamini yasiyoonekana na husimamisha Sala na hutoa katika yale Tuliyowapa. Enyi mlioamini, toeni katika vile Tulivyowapeni kabla haijafika siku ambayo haitakuwa na

biashara, wala urafiki wala uombezi; na waliokufuru ndio wadhalimu. (2:4, 255).
(Na wafanyao wema ni) watoao katika (hali ya) faraja na dhiki na wazuiao ghadhabu na kuwasamehe watu; na Mwenyezi Mungu Hupenda wafanyao ihsani. (3:135).
Hakuna heri katika mengi wanayoshauriana kwa siri, isipokuwa (mashauri ya) yule anayeamuru kutoa sadaka au kufanya wema au kupatanisha baina ya watu; na atakayefanya hivi kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, basi hivi karibuni Tutampa ujira mkubwa. (4:115).
Na ambao husubiri kwa kutaka radhi ya Mola wao, na wakasimamisha Sala na wakatoa katika vile Tulivyowapa, kwa siri na dhahiri, na kuyaondoa maovu kwa wema, hao ndio watapata malipo (mema) ya nyumba (ya Akhera). (13:23).
Waambie watumishi Wangu walioamini, wasimamishe Sala, na watoe katika vile Tulivyowaruzuku kwa siri na dhahiri kabla haijafika siku isiyo na biashara wala urafiki. (14:32).
Mwenyezi Mungu Anapiga mfano wa mtumwa anayemilikiwa asiyeweza cho chote; na (mwingine) Tuliyemruzuku kutoka kwetu riziki njema, naye anatoa katika hiyo kwa siri na dhahiri, je, wako sawa? Alhamdulillahi! lakini wengi wao hawajui. (16:76).
Kwa yakini wale wanasoma kitabu cha Mwenyezi Mungu, na wanasimamisha Sala, na katika yale Tuliyowapa wanatoa kwa siri na kwa dhahiri, wanatumai bishara isiyoangamia.
(35:30).
Na wale waliomwitikia Mola wao, na husimamisha Sala, na sharia yao ni kushauriana wao kwa wao, na hutoa katika yale Tuliyowaruzuku. (42:39).
Mwaminini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na toeni katika yale Aliyowakabidhini. Basi wale walioamini miongoni mwenu wakatoa, wana malipo makubwa. (57:8).
Na toeni katika yale Tuliyowapeni kabla mmoja wenu haijamfikia mauti, kisha aseme: Mola wangu, mbona hukuniakhirisha muda kidogo, nikatoa sadaka na nikawa miongoni mwa watendao mema? (63:11).
Kwa hiyo mcheni Mwenyezi Mungu mwezavyo, na sikilizeni na tiini na toeni, itakuwa heri kwa nafsi zenu; na aepushwaye na ubahili wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufaulu. (64:17).

**UBORA WA KUTOA SADAKA**

Mfano wa wale wanaotoa mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu, ni kama mfano wa punje moja itoayo masuke saba katika kila suke punje mia. Na Mwenyezi Mungu Humzidishia Amtakaye; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua.
Shetani anawaogofisheni ufukara na anawaamuruni ubahili, na Mwenyezi Mungu Anawaahidini msamaha utokao Kwake na ukarimu; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua,
Na cho chote mtoacho au nadhiri mnazoweka, basi hakika Mwenyezi Mungu Anazijua; na kwa wadhalimu hawatakuwako wasaidizi.
Kama mkitoa sadaka kwa dhahiri ni vizuri; na kama mkitoa kwa siri na kuwapa mafakiri, basi huo ni ubora kwenu; na Atawaondoleeni sehemu ya maovu yenu; na Mwenyezi Mungu anazo habari za yale mnayoyatenda.
Kwa (kuwapa) mafakiri waliozuiwa katika njia ya Mwenyezi Mungu, wasioweza kutembea huko na huko katika ardhi; mjinga anawadhani ni matajiri kwa sababu ya kujizuia (kuomba). Utawafahamu kwa alama zao; hawaombi watu kwa ung'ang'anizi.
Na mali yo yote mnayotoa, basi kwa yakini Mwenyezi Mungu Anaijua.
Wale watoao mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhahiri, basi wana ujira wao kwa Mola wao; wala haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika.
Mwenyezi Mungu Hufuta riba na Hukuza sadaka, na Mwenyezi Mungu Hampendi kila kafiri afanyaye dhambi.
Hakika wale walioamini na kufanya vitendo vizuri na kusimamisha Sala na kutoa Zaka, wao watapata ujira wao kwa Mola wao, wala haitakuwa hofu juu yao, wala hawatahuzunika.
(2: 262, 269, 271, 272, 274, 275, 277, 278).
Sema: Kwa hakika Mola wangu Humnyoshea riziki amtakaye katika watumishi Wake, na Humdhikisha. Na cho chote mtakachotoa, basi yeye atakilipa; naye ni Mbora wa wanaoruzuku.
(34 :40).

**MWENYEZI MUNGU APOKEA SADAKA**
Je, hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu ndiye Anayepokea toba ya watumishi Wake na kuzipokea sadaka, na ya kwamba Mwenyezi Mungu Hupokea toba, Mwenye rehema. (9:104).

**UBAYA WA UBAHILI**
Shetani anawaogofisheni ufukara na anawaamuruni ubahili, na Mwenyezi Mungu Anawaahidini msamaha utokao Kwake na ukarimu; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua. (2:269).

Wala wasione wale ambao wanafanya ubahili katika yale Aliyowapa Mwenyezi Mungu katika fadhili Zake kuwa ni bora kwao; la, ni vibaya kwao; watafungwa kongwa za yale waliyoyanyia ubahili siku ya Kiyama; na urithi wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu Ana habari za mnayoyafanya. (3: 181).
Na Mwabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na cho chote, na wafanyieni hisani wazazi na pia jamaa za ukoo, na yatima na maskini na jirani miongoni mwa jamaa, na jirani ambaye si jamaa, na rafiki aliye kando (yako), na msafiri, na wale iliyowamiliki mikono yenu ya kiume; bila shaka Mwenyezi Mungu Hampendi mwenye kiburi, ajivunaye.
Hakika Mwenyezi Mungu Hadhulumu (hata sawa na) uzito wa chembe; na kama likiwa ni tendo jema, Yeye Atalizidisha na kutoa ujira mkubwa kutoka Kwake. (4:37,41).
Enyi mlioamini! bila shaka wengi katika makasisi na wamonaki wanakula mali za watu kwa batili na kuwazuilia njia ya Mwenyezi Mungu. Na wale wakusanyao dhahabu na fedha wala hawazitoi katika njia ya Mwenyezi Mungu, basi wape habari za adhabu iumizayo. (9:34).
Lo! ninyi ndio mnaitwa ili mtoe (mali) katika njia ya Mwenyezi Mungu, lakini wengine wenu wanafanya ubahili; na afanyae ubahili basi hakika anafanya ubahili kwa (kuidhuru) nafsi yake. Mwenyezi Mungu ni Mkwasi nanyi ni mafakiri. Na kama mkirudi nyuma basi Mwenyezi Mungu Ataleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa mfano wenu. (47:39).

**UBAYA WA UDHIA NA KUSIMBULIA**
Kauli njema na msamaha ni bora kuliko sadaka inayofuatishwa na udhia; na Mwenyezi Mungu ndiye Mkwasi, Avumiliaye.
Enyi mlioamini, msiharibu sadaka zenu kwa masimbulizi na udhia, kama yule anayetoa mali yake kuwaonyesha watu, wala hamwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Basi hali yake ni kama hali ya mwamba juu yake kuna udongo, kisha ikaufikia mvua kubwa na ikauacha mtupu; hawatakuwa na uwezo juu ya cho chote katika wanavyovichuma; na Mwenyezi Mungu Hawaongozi watu makafiri. (2: 264, 265,).

**HADITHI ZA MTUME S.A.W.**
1. Mtume s.a.w. alikuwa akisema, “Zaka ndilo daraja la Uislamu.” Yaani humtoa mtu katika shida na kumwingiza katika neema.
2. Na pia alikuwa anasema, “Aliyetoa Zaka katika mali yake, basi yeye ameepuka ubaya wake.”
3. Akasema tena, “Zilindeni mali zenu kwa kutoa Zaka na ponyesheni magonjwa yenu kwa sadaka.”
4. “Mtu ye yote asiyetoa Zaka mali yake, ataletewa mali yake Siku ya Kiyama kwa sura ya joka lenye upara (mkali wa sumu) nalo litazunguka shingo lake kama mkufu.” .
5. “Mali haipotei barani au baharini ila kwa kuzuia Zaka.”
6. “Umati wo wote wa, watu hauzuii Zaka ila wananyimwa mvua; na lau kama si wanyama hawangeteremshiwa mvua kamwe.”
7. “Mtume s.a.w. alihimiza watu siku moja kutoa sadaka, basi watu wakaanza kutoa papo kwa papo. Akajitokeza mtu mmoja aliyekuwa na nguo mbili tu, hakuwa na nyingine, akatoa moja. Mtume s.a.w. akamrudishia, ila akasema, wewe ndiwe una haki zaidi juu yake.”
8. “Mtume s.a.w. alikuwa anasema, “Pengine unalazimika kutoa sadaka, lakini hutoi, basi

haramu inaangamiza mali yako ya halali. Bila shaka haramu haichanganyiki na halali ila inaihilikisha."

9. Mtume s.a.w. alipoletewa sadaka na mtu ye yote alikuwa anamwombea baraka.

10. "Sadaka iliyotolewa kwa kumpa maskini aliye jamaa ina thawabu mara mbili; thawabu ya sadaka na thawabu ya kusaidia jamaa." ,

11. Mara nyingi Mtume s.a.w. aliwapa washirikina mali ya sadaka.

12. Mtume s.a.w. alisema, "Siku Mwenyezi Mungu aliyoumba ardhi, ilianza kuyumbayumba. Mwenyezi Mungu akaweka milima juu yake, ikatulia.

Malaika walistaajabu sana kwa ugumu wa milima, wakamwuuliza Mwenyezi Mungu, Je, Umeumba kitu kilicho kigumu kuliko hiyo? Akasema, 'Chuma'. Wakauliza Je, kuna kitu kinachoshinda Chuma? Akasema, 'Moto'. Wakauliza, Je, kuna kitu kinachoshinda moto? Akasema, 'Maji'. Tena wakauliza, Nini chashinda maji? Akasema, 'upepo'. Wakauliza tena, Kuna kitu chenye kupita upepo? Mwenyezi Mungu akajibu, Sadaka ambayo hutolewa kwa mkono wa kulia na hali mkono wa kushoto haupati habari yake." (Yaani sadaka inayotolewa kwa kuficha).

# SAUMU YA RAMADHAN

Saumu ya mwezi wa Ramadhani ndio nguzo ya nne ya Dini ya Kiislamu. Saumu ni neno la Kiarabu, na maana yake ni kuacha. Na katika sheria ya Kiislamu neno hilo limekuwa na maana ya kuacha kula na kunywa na kufikiliana na wake, toka mapambazuko mpaka kutua jua.

**SAUMU ILIANZA LINI?**

Kufunga saumu ni desturi ya tangu na tangu. Kurani yenyewe imekwisha tuambia "Mmelazimishwa kufunga saumu kama walivyolazimishwa wale wa kabla yenu ili mpate
kujilinda." Toka kabla ya Uislamu watu wa kila dini walikuwa wanafunga saumu. Mabaniani, Mayahudi na Wakristo wote wanazo saumu za namna zao. Kadhalika dini zile zilizofutika, kama dini za Waselti, Watuto, Wamekisiko, Waperuvi, Wababili, Waasuria, Wamisri wa kale, Warumi na Wagiriki wote hao walikuwa na kanuni za kufunga saumu.
Yesu Kristo (Nabii Isa) pia alifunga saumu. Lakini kwa kuwa dini hii ilikusudiwa na Mwenyezi Mungu ifutike, basi Yesu hakueleza habari nyingi zinazohusu saumu. Na kwa sababu hii Wakristo wamekuwa na namna za saumu za kujibunia wenyewe: hapo kwanza kulikuwa na Wakristo ambao walipofunga saumu waliacha kabisa kula na kunywa. Wengine wao hivi leo, kufunga kwao ni kula chakula kidogo kidogo pasipo kushiba, na wengine hufunga wasile nyama tu, au mboga tu, au kitu fulani chochote na vinginevyo wakajilia.
Dini ya Islam imetuwekea kanuni zilizo bora za saumu ambazo hazipatikani katika dini zingine. Ndio kusema dini yetu imekamilisha ibada hii na kuifanya iwe na faida kubwa ya kiroho kwa ajili ya wafuasi wake. Haya maelezo tuliyoandika juu ya saumu hayapatikani katika vitabu vya dini nyinginezo.
Basi kufunga saumu si amri mpya kuletwa na Uislam kama alivyokwisha sema Mwenyezi Mungu mwenyewe. Amri hii ya kufunga saumu ilishuka kwa Waislamu katika mwaka wa pili wa Hijra, yaani miaka miwili baada Mtume (s.a.w.) kuhajiri na kwenda kaa Madina.
Kuna Waislamu wengine wasio na habari kamili ya Dini Ya Kiislamu wanaofikiri ya kuwa saumu ilifaradhiwa kwa Waarabu wa zamani ambao walikuwa wakila ovyo, ndipo ikaletwa amri ya saumu; lakini kwa watu waliostaarabika wa siku hizi saumu si kitu cha lazima. Fikira hii ni ya upotovu sana wala haina dalili hata nusu. Na kama tukiacha kufuata amri za dini yetu kwa sababu ya mawazo yetu tu, basi tutajipeleka mbali sana na Uislamu. Juu ya kila amri ya Kurani Tukufu hoja mbovu kama hiyo inaweza kuletwa ya kusema kwamba agizo hili lilikusudiwa kwa ajili ya Waislamu wa zamani sio sisi wa karne ya 20. Hazrat Seyidna Ahmad A.S. ambaye ameletwa na Mwenyezi Mungu katika karne hii ili kung'oa fikira zilizopotoka amesema wazi wazi ya kuwa kufunga saumu katika mwezi wa Ramadhani ni jambo la faradhi kwa kila Mwislamu. Basi watu walio na mawazo kinyume cha hayo wajisahihishe na watubu dhambi zao na walipe saumu zote walizopoteza katika miaka iliyopita.

**MAAGIZO YA KURANI TUKUFU JUU YA SAUMU.**

Mwenyezi Mungu amesema katika Kurani, "Enyi mlioamini, mmelazimishwa kufunga saumu kama walivyolazimishwa wale wa kabla yenu ili mpate kujilinda, kwa siku zilizohesabiwa; lakini awaye mgonjwa miongoni mwenu au katika safari alipe katika siku zingine; na wale wenye uwezo watoe fidia kwa kumlisha maskini, na atakayefanya wema kwa radhi ya nafsi yake basi ni bora kwake na kama mkifunga saumu ni bora zaidi kwenu ikiwa mnajua."
Mwenyezi Mungu amesema katika Kurani Tukufu juu ya mwezi wa Ramadhan ya kuwa:-

Yaani: "Mwezi wa Ramadhan, ambao humo imeteremshwa Kurani kuwa mwongozo kwa watu na dalili zilizo wazi na mwongozo na ishara ipambanuayo. Na miongoni mwenu atakayeuona mwezi huu basi afunge saumu. Na awaye mgonjwa au katika safari basi alipe katika siku zingine. Mwenyezi Mungu huwatakieni yaliyo mepesi wala hawatakieni yaliyo mazito, na pia huwatakieni mtimize hesabu na kumtukuza kwa sababu amewaongozeni, ili mpate kushukuru." (2: 184, 185. 186).
"Na watu Wangu watakapokuuliza juu Yangu, basi Mimi niko karibu, nayaitikia maombi ya mwombaji

anaponiomba, hivyo waniitikie na waniamini ili wapate kuongoka. Mmehalalishiwa usiku wa saumu kuingiliana na wake zenu; wao ni nguo kwenu na ninyi ni nguo kwao. Mwenyezi Mungu ajua kwamba mlikuwa mkijihini nafsi zenu kwa hiyo amewaelekeeni na kuwasameheni. Basi sasa fikilianeni nao na takeni aliyowaandikieni Mwenyezi Mungu, na kuleni na kunyweni mpaka upambanuke kwenu uzi mweupe wa alfajiri katika uzi mweusi (wa usiku); kisha timizeni saumu mpaka usiku wala msiingiliane nao na hali mnakaa I'tikaaf msikitini. Hiyo ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu, basi msiikaribie. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu hubainishavyo ishara Zake kwa watu ili wapate kujilinda." (2: 187-188).

**SIKU ZA SAUMU.**

Siku za saumu zilizolazimishwa ni mwezi wa Ramadhani. Mtume (s.a.w.) amesema, "Fungeni kwa kuona mwezi na fungueni kwa kuuona mwezi" (Bukhari). Siku 6 za Shawwal na saumu zingine hazikulazimishwa: anayefunga anapata thawabu na asiyefunga hapati dhambi. Imekatazwa kufunga ili kuulaki mwezi kama wafanyavyo watu wengine wenye shauku wakiona umekaribia mwezi wa Ramadhani wanaanza kufunga wakisema wanajiweka tayari ili kuupokea. Kufunga kwa namna hii kumekatazwa na Mtume (s.a.w.) Kadhalika kuna watu wasiojua ambao hupenda kuendelea na saumu zao, hawafungui siku ya Idi mpaka kumaliza siku 6 za Shawwal.
Jambo hili la kufunga siku ya Idi ni baya sana, hata Mtume (s.a.w.) akasema ya kuwa anayefunga siku ya Idi, basi amekuwa shetani. Hata kama mtu anazo saumu za kulipa, itamlazimu asifunge siku ya Idi, bali ale na afunge katika siku zifuatazo.

**SAUMU YA MGONJWA.**

Mgonjwa au mtu aliyomo safarini ameambiwa na Mwenyezi Mungu afunge katika siku zingine za afya na baada ya kutoka safarini. Hadi ya ugonjwa ni kiasi cha mtu kujifahamu kuwa yu mgonjwa, basi asifunge; maana akifunga naye ni mgonjwa, amevunja amri ya Mwenyezi Mungu isemayo mgonjwa afunge siku zingine. Lakini basi mtu anatakiwa kutumia akili pia. Ugonjwa sio maana yake mtu anaumwa umwa kidole au mavune ya mchoko au udhia mwingine mdogo mdogo. Ama kwa kutapika saumu haivunjiki isipokuwa mtu ajitapishe kusudi. Wakongwe na wadhaifa wa daima wamepewa ruhusa wasifunge, wakiweza wamlishe maskini mmoja kila siku ya saumu. Mwanamke mwenye mimba au anayenyonyesha akihofia dhara juu yake au juu ya mtoto, asifunge.
Atoe fidia kwa kumlisha maskini kila siku ya saumu au alipe funga katika siku zingine. Mwanamke mwenye hedhi alipe kwa kufunga siku zingine.
Baadhi ya watu hawana hakika kama katika hali ya saumu mtu anaweza kupigwa sindano au hapana na akipata sindano saumu itasihi au itaharibika. Ukweli wake ndio huu ya kuwa mgonjwa hana saumu. Na ikiwa anaugua kiasi cha kuhitaji kupigwa sindano, basi bila shaka yeye atatakiwa kutii amri na kufuturu hata kama hakupigwa sindano. Na kama anapigwa sindano si kwa sababu ya maradhi bali kwa satabu nyingine, kama kutaka cheti cha kusafiria (passport), hata hivyo saumu yake itabatilika kwani dawa inaingizwa mwilini. Kadhalika damu ikiingizwa mwilini saumu inaharibika vile vile ingawa damu haiingii tumboni, bali mishipani.
Hadi ya safari ni ile inayosemwa safari. Watu wengine kwa kukosa kujua husema, safari ya mashine na safari ya ndege si safari za taabu na kama mtu katika hali ile afunge saumu si vibaya. Hii ni kosa, Mtume (s.a.w.) amesema, "Si wema kufunga saumu katika safari" [Bukhari]. Mungu hawi radhi kwa kushurutishwa, bali anakuwa radhi yakifuatwa anayoagiza. Hivyo mtu na awe na raha ya namna gani katika safari lazima asifunge, na akimaliza safari alipe siku alizokula; kwani Mwenyezi Mungu aliyelazimisha saumu ni Mjuzi wa kila kitu, na alijua zitakuwapo safari za raha mbona basi asiseme katika safari za raha mfunge? Watu wengine hufunga katika safari wakiogopa taabu ya kufunga peke yao baadaye. Basi wajue ndivyo hivyo alivyowatakia Mungu wawe safarini, ili wafunge saumu huku wakishawishiwa na ulaji wa watu wengine wasiofunga.
Sheria yetu haikatazi watu wasisafiri katika mwezi wa Ramadhan. Bali yameandikwa katika vyuo vya Hadithi kuwa Mtume wetu s.a.w. naye alipata kusafiri mara nyingi katika mwezi mtukufu wa Ramadhani. Naam katika safari hizo alikuwa hafungi saumu. Na kama aliondoka kwa ajili ya safari hali ana saumu, basi akifika nje ya mji akafuturu. Wakati mwingine alikuwa anaagiza kikombe cha maji akayanywa mbele ya watu wote ili wale walio na saumu kati yao

wafuturu pia.
Imeandikwa katika Sahih Muslim ya kuwa siku moja Mtume s.a.w. alitoka nyumbani hali amefunga saumu. Alipofika mahali panapoitwa Kura'al Ghamim, umbali wa maili nane, akaagiza maji ya kunywa. Alipoletewa maji ndani ya kikombe alikiinua juu sana ili watu wengine wapate kuona vizuri tendo lake. Kisha akanywa maji hayo hadharani. Baadaye Mtume S.A.W. aliambiwa ya kuwa baadhi ya watu waliokuwa pamoja na Mtume s.a.w. hawajafuturu. Kusikia hivi Mtume s.a.w. akakasirika na akasema: "Hao ndio waasi, hao ndio waasi."
Ni kweli kuna hadithi nyingine zinazoeleza ya kuwa hata katika hali ya safari mtu anaweza kufunga na saumu yake ikasihi; lakini katika Sahih Muslim mna hadithi iliyopokelewa na Ibni Abbas, radhi ya Mwenyezi Mungu iwe kwake inayosema ya kwamba desturi ya Mtume s.a.w. katika miaka ya mwisho wa uhai ilikuwa kutofunga saumu aliposafiri katika mwezi wa Ramadhan na hii ndiyo desturi iliyoshikwa na Masahaba wote waliopenda kufuata desturi ya mwisho ya Mtume s.a.w. Hivyo kufunga saumu katika safari ni kinyume cha desturi (sunna) ya Mtume s.a.w. kama ilivyo kinyume cha maagizo ya Kurani Tukufu. Naam, ni lazima saumu hizi zilizofutu zilipwe baadaye katika miezi iliyofuata. Na mwenye kuacha kufunga atapata dhambi.

**DAKU**
Watu wa nchi hii wanakula daku saa sita usiku. Hii sio desturi ya Kiislamu bali ni mwendo wa Mayahudi. Waislamu wameambiwa na Kurani Takatifu na Mtume Muhammad s.a.w. wale daku saa kidogo kabla ya kubainika alfajiri, ndio sunna ya Mtume s.a.w. Kabla ya kula daku watu wanatakiwa kuamka na kusali sala ya Tahajjud na kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kisha wale daku karibu ya alfajiri.

**FUTARI.**
Mara jua likitua inatakiwa kufuturu mara moja. Mtume (s.a.w.) amesema, "Waislamu kama watafanya haraka kufuturu wataendelea katika kheri". (Bukhari). Wakati wa kufuturu inatakiwa kuomba dua hii: *Allahumma laka sumtu Wa'alaa rizkika aftartu.* Maana yake, Ee Mola wangu, nimefunga saumu kwa ajili Yako na kwa riziki Yako naifungua. Kukawia kufuturu hakupendezi. Sababu ni wazi. Anayefuturu upesi anafuata amri ya Mungu, na kufuata amri ya Mungu ndio njia ya kheri. Lakini anayekawia kufuturu anafuata matamanio yake, na njia hii humkasirisha Mungu.
Neno hili "futari" maana yake ni kitu cho chote anachokula mtu anapofungua saumu wakati wa jioni. Na kwa kuwa watu wa nchi hii hupeda kufuturu kwa chakula kilicho laini basi hutumia mchanyato wa viazi au ndizi, muhogo na vinginevyo; hata wasio na habari wamekwisha dhani ya kuwa mchanyato tu ndio futari. Na wengine hudhani huu mchanyato asipokuwa nao, basi hana lazima ya kufunga: husema, "Mimi sikufunga maana sina futari" yaani hana mchanyato na hali hata ugali au maji au kulamba chumvi mtu anaweza kufanya ndio futari yake. Kadhalika wapo wengine wanaodhani kuwa saumu haiwi kamili mpaka mtu aanze kufuturu kwa uji. Jambo hili si kweli! Pana uchafu hapa unaotakiwa kuelezwa. Hakuna Mwislamu asiyejua ya kuwa ni haramu kabisa mwanamke na mwanamume wasiofunga ndoa na kuoana kukaa kinyumba. Jambo hili ni haramu kabisa siku zote. Lakini inasikitisha kuona watu wanaojiita Waislamu siku hizi hawaoni hata haya kuweka vimada, na wanadhani vimada wao wameharimishwa si kwa shauri lingine ila kwa kupika uji wa mwezi wa Ramadhani! Wanasema, bibi zao wana haki kupika vyakula vingine isipokuwa uji katika mwezi huu. Fikira hizi ni chafu kabisa na ni ujahili mtupu! Je, haujafika wakati watu hao wakamcha Mungu na kuacha uchafu huu? Basi jueni kuweka vimada mwezi wa Ramadhani na kujidai mtu anafunga ni kazi bure, hata kama mwanamke huyo akapika au asipike uji mamoja - yote mawili ni haramu.

Kadhalika wakati wa kufuturu mtu anatakiwa ale kwa kiasi. Mwenyezi Mungu anasema, "Kuleni na kunyweni wala msizidi kiasi, hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wanaozidi kiasi (7; 32). Kula sana kunamfanya mtu awe mvivu na aone uzito kuamka katika ibada za usiku.

**MAMBO MENGINE YANAYOHUSU SAUMU**

Mtu anapokuwa na saumu kama haachi mambo mabaya na kusema uwongo basi hali yake ni sawa na mtu aliyekaa na njaa tu. Katika siku za saumu mtu anatakiwa apitishe mchana na usiku katika ibada na mambo mema na maneno mazuri, kusoma Kurani na kuwasaidia maskini na mafukara. Kama mtu amtukane asimrudishie tusi na kugombana naye ila amwambie: Tafadhali niache, nina saumu.

Katika hali ya saumu mtu anaweza kupiga mswaki, kuoga na kujipaka manukato (Bukhari).

Katika hali ya saumu mtu hana ruhusa kuvuta sigara au kunusa tumbaku au kuitia mdomoni.

Mwanamke anayemwogopa mumewe anaweza kuonja chumvi katika chakula kwa ulimi tu, asiimeze, Katika usiku wa saumu mtu anayo ruhusa kuingiliana na mkewe (Kurani).

Mtu aliyefunga akila na akinywa kwa kusahau, saumu yake haikuvunjika (Bukhari).

Watoto hawakulazimishwa kufunga saumu, Kuwashurutisha si vizuri. Mahali pengine watoto wamepata kufa kwa kulazimishwa kufunga. Kama watoto wamekuwa na umri mkubwa kidogo wafundishwe hakika na faida ya saumu.

**I'TIKAAF**

Siku 10 za mwisho wa Ramadhan kama mtu anaweza kukaa katika msikiti mchana na usiku na kufanya ibada ndio sunna ya Mtume (s.a.w.) na inaitwa l'tikaf. Katika hali ya I'tikaf mtu hana ruhusa kuingiliana na mke wala kwenda nyumbani wala kutembea tembea wala kutoka isipokuwa kwa haja ya choo tu, Akae msikitini tu na kufanya ibada, Wanawake pia wanaweza kukaa msikitini mahali pao mbali na wanaume.

**LAILAT-UL-KADRI.**

Mungu amesema katika Kurani ya kwamba Lailat-ut-Kadr ndio usiku ulio bora kwa kheri kuliko miezi elfu. Mtume (s.a.w.) akasema, "Usiku huu hutokea katika siku 10 za mwisho wa Ramadhan katika usiku mmojapo katika tarehe 21, 23, 25, 27 na 29" (Bukhari). Tena Mtume (s.a.w.) amesema kuwa kama mtu anafanya ibada katika usiku huu kwa imani na kutumaini, dhambi zake zote zilizotangulia zinasamehewa.

**SADAKA YA FITRI**

Mtume (s.a.w.) amewalazimisha Waislamu wote wanawake kwa wanaume, hata watoto wachanga, watoe sadaka ya fitri, kila mmoja ratili 8 za nafaka. Kwa mfano, baba na mama na watoto watatu wote pamoja ni watu watano; kwa kila mtu ratili 8 watatoa ratili 40. Ikiwa hawana nafaka watatoa fedha yenye thamani ya ratili hizi. Lakini maskini na wasio na uwezo watatoa nusu. Sadaka hii hupelekwa kwa mkubwa wa Waislamu wa mahali alipo naye atagawia maskini na mafukara kabla ya siku ya Idi ili nao wajinunulie nguo mpya na kujifurahisha katika siku kuu ya Idi.

**HEKIMA ZA SAUMU**

Faida za saumu ni nyingi, chache ni hizi:-

(1) Kama alivyosema Mwenyezi Mungu, *la'allakum tattakun,* yaani, ili mpate kumcha Mungu. Ndio kusema ya kuwa anayefunga anajilinda roho na kiwiliwili na anaepuka madhambi na maradhi. Mtume (s.a.w.) akasema "Fungeni saumu mpate afya." Jambo hili linajulikana sana kwa watu wenye elimu ya kuwa kufunga saumu kunampa mtu afya na kumpa uwezo wa kujizuia anaposhambuliwa na mawazo na mashawishi mabaya. Kadhalika wako madaktari waliochungua na kuhakikisha ya kuwa mtu anaweza kupona magonjwa mengi kwa kufunga saumu.

(2) Imehimizwa kulisha masikini katika siku za saumu na tunahadithiwa kuwa Mtume (s.a.w.) juu ya ukarimu wake ajabu alizidi sana mwezi wa Ramadhani. Waswahili wanasema, "Mwenye

shibe hajui njaa ya mwenziwe." Lakini Waislamu wenye shibe na matajiri wamekwisha fundishwa kuona njaa pamoja na maskini. Hivyo njaa si kitu kigeni
kwao, na kwa hivyo kila mara wanawaonea maskini huruma kwa njaa yao na wanawasaidia.

(3) Mwenyezi Mungu anataka kumfundisha Mwislamu si kwa maneno tu bali kwa matendo pia; ni kama kumwambia, Ewe Mwislamu katika mwezi huu wa Ramadhani umekuwa radhi kuacha kula na kunywa hata vitu vilivyo halali kwa ajili yangu Mimi Mola wako. Hivyo, si vigumu kwako kuacha kabisa vitu vyote vibaya vitavyokudhuru ambavyo ninakukataza, ikiwa utatii maagizo Yangu ninayokuamrisha.
Basi hakika ya saumu si kuacha kula na kunywa tu, bali Mwislamu anatakiwa afunge saumu ya macho asitazame ila vilivyoruhusiwa; afunge masikio asisikilize ila yanayompasa;
afunge kinywa asiseme ila ukweli na yaliyo kheri. Ajitupe kabisa kwa Mwenyezi Mungu. Na Seyidna Ahmad Masihi na Mahdi aliyeahidiwa amesema, "Kamilisheni sawasawa saumu zenu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu" (Safina ya Nuhu).
(4) Kwa desturi watu hawakumbuki jumla ya neema za Mwenyezi Mungu walizo nazo mpaka zinapowatoka. Kwa mfano, macho ni kitu cha thamani sana, lakini watu hawakumbuki zaidi thamani yake ila wanapopotewa na macho yao. Hivyo mtu atakapoona njaa na kiu, atakumbuka kushukuru neema nyingi za Mwenyezi Mungu alizo nazo na atakuwa mtu mwema.
(5) Mwislamu kwa kufunga saumu anafundishwa kukaa tayari kupambana na dhiki, na kuwa radhi kujinyima. Itakapotokea haja ya kusaidia dini au kusaidia taifa asianze kuona mbona shibe yangu inapungua; bali awe tayari kuvumilia taabu na kujinyima ili mahitaji ya Dini na taifa yatimie. Ni wazi kabisa mtu aliyezoea kushinda na njaa mwezi mzima-mzima anapolazimika kubeba mashaka ya njaa na taabu huwa na subira zaidi kuliko mwenziwe asiyekuwa kama yeye.

## SALA YA IDI

Utakapoonekana mwezi wa Mfungo mosi (Shawwal) basi Ramadhani itakwisha na tarehe ya kwanza itakuwa siku ya Idi. Idi hii inaitwa Id-ul-Fitri. Waislamu wanatakiwa kuoga na kuvaa nguo safi na kutumia mafuta mazuri na waende kusali kwa kupita katika njia moja na warudi kutoka kusali wanapokwenda nyumbani kwa kupita katika njia nyingine. Baada ya Sala ya Alfajiri mpaka Sala ya Idi hakuna Sala yo yote ya nafali au sunna, imekatazwa kabisa. Imam atasalisha kwanza rakaa mbili na katika rakaa ya kwanza baada ya takbira ya kwanza atasema takbira zingine saba na maneno katika kusali ni yale yale yanayotumiwa katika sala za kawaida. Katika rakaa ya pili baada ya kusema Allahu Akbar mara ya kwanza zitasemwa takbira zingine tano na zote jumla ni takbira sita. Tena Imam atasoma sura Alhamdu na sura moja nyingine kwa sauti kubwa kama inavyosomwa katika sala za Ijumaa na sala zingine. Sala itakapokwisha Imam atatoa hotuba. Hakuna Adhana wala Ikamat katika sala ya Idi.
Siku hii ya Idi ni siku ya furaha waliyopewa Waislamu na Mwenyezi Mungu ili wapate kujifurahisha kama anavyofurahi mtu baada ya kupewa kazi ngumu iliyo kubwa na akaimaliza kwa ufaulu. Hivyo Waislamu katika siku hii humtukuza na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwapa uwezo wa kuumaliza mwezi wa Ramadhani ulio na neema kwa kufanikiwa. Basi ni wale hasa waliojitahidi kutekeleza sawasawa sharti za saumu wanaostahili sehemu kubwa zaidi ya furaha hasa ya siku hii tukufu. Idi ni kwa yule aliyemcha Mungu sawasawa akajiepusha na kila maovu na kujilazimisha katika wema na utii kamili katika mwezi huu mtukufu: si Idi kwa avaaye nguo nzuri katika siku hiyo ambaye hakuwa na lo lote ila kiu na njaa tu katika mwezi huo uliotukuzwa.